TANGAZO LA SERIKALI Na. 104 la tarehe 16/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA SANGAMBI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Sangambi ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

**JEDWALI**

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MJ1 yenye majira-nukta 565066.558MS, 9053226.812KZ; baada ya hapo mpaka unelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa 56º48′44″ kwa umbali wa kilomita 1.67 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MJ2 yenye majira-nukta 563670.746MS, 9054139.784KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki kwa kufuata uelekeo wa 25º07′53″ kwa umbali wa kilomita 1.02 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MJ3 yenye majira-nukta 564102.694MS, 9055060.577KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa 37º16′05″ kwa umbali wa kilomita 1.82 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SANG2 yenye majira-nukta 565202.027MS, 9056505.327KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa 06º16′58″ kwa umbali wa kilomita 1.38 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SANG3 yenye majira-nukta 565050.881MS, 9057878.188KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa 23º07′36″kwa umbali wa kilomita 1.08 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SANG4 yenye majira-nukta 565474.299MS, 9058869.596KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa 84º05′39″ kwa umbali wa kilomita 1.96 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SANG5 yenye majira-nukta 567420.659MS, 9058668.261KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa 35º33′55″ kwa umbali wa kilomita 1.38 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SANG6 yenye majira-nukta 568220.608MS, 9057549.477KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa 43º24′14″ kwa umbali wa kilomita 1.66 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SANG1 yenye majira-nukta 567077.913MS, 9056341.27KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa 28º59′41″ kwa umbali wa kilomita 2.64 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MJ5 yenye majira-nukta 565796.08MS, 9054028.289KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa 05º22′06″ kwa umbali wa kilomita 1.48 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*